Toleo Nam. 001 / Mei 2019 / Haliuzwi

# ZURA

ZURA
Zanzibar Utilities Regulatory Authority

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar



## ZURA Kuingia katika ushindani Duniani - Uk.7

Email:info@zura.go.tz / Facebook: zura / Instagram:zura_mamlaka / Twitter:zura_znz / Website:www.zura.go.tz

## Bodi ya Wahariri

**Mhariri Mkuu:**
Dk. Ally S. Mwinyikai

**Msaidizi Mhariri Mkuu:**
Khatib H. Khatib

**Waandishi:**
Khuzaimat Bakar Kheir
Mbarak Hassan Haji

**Mpiga Picha:**
Hassan Juma Amour

**Msanifu:**
Aziz Iddi Suwedi

**Msambazaji:**
Mwinyi Ahmed Mwinyi


## UTAMBULISHO

Jarida hili limeandaliwa ili kuwapa fursa wananchi kufahamu majukumu ya Mamlaka ya Uthibiti ya Huduma za Maji na Nishati, Zanzibar (ZURA) na utekelezaji wa kazi zake za kila siku.

ZURA katika kazi zake inakusanya sekta ya maji, mafuta, umeme na gesi a mbazo zote zina umuhumu makubwa katika maisha ya binadamu. Hivyo, Jarida hili linahitaji kupata ushirikiano kutoka kwa wananchi kwa lengo la kuikuza na kuiendeleza ustawi na maendeleo ya jamii kwa faida ya wananchi na Taifa kwa jumla.

Ushirikiano wenye tija ni ule utakaowafanya wananchi kutoa michango yao katika kuliendeleza Jarida hili kwa mtindo wa Makala, habari, picha na maoni ili kutimiza lengo lililokusudiwa la kuwa daraja la kuwaunganisha wananchi katika kuhakikisha huduma bora za maji na nishati.

Jarida hili, linategemea sana mawazo, fikra, maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau kupitia njia tofauti za mawasiliano kutoka sehemu mbalimbali za Zanzibar.


P.O. Box 2238
Zanzibar- Tanzania
Simu: +255 24 223 8316
Eax: +255 24 223 8317
Email: info@zura.go.tz


## MAONI YA MHARIRI

# Jarida la ZURA lazaliwa

KWA kawaida mtoto anapozaliwa huhitaji matunzo na malezi mema kutoka kwa wazazi wake na pia jamii inayomzunguka. Wazazi na jamii huweka matarajio makubwa kutokana na kizaliwacho na hivyo kulazimika kuwekeza kwa kadiri inavyowezekana ili kufikia matarajio yao.

Kuzaliwa kwa mtoto – Jarida la ZURA ni mwanzo mzuri wa kuonesha dhamira njema ya kushirikiana baina ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar na wadau wote wanaotoa, wanaopatiwa na wanaohitaji huduma zinazotokana na sekta ya Maji na Nishati.

Jarida hili lililoasisiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar, lina malengo maalumu ya kuwapatia taarifa muhimu wananchi kuhusiana na masuala ya maji na nishati kwa jumla.

Mategemeo makubwa ya Mamlaka ni kwamba Jarida hili litapokelewa na wananchi na kuendelea kutoa ushirikiano wao kikamilifu katika kuikuza na kuiendeleza Mamlaka hiyo kwa faida yao na Taifa kwa jumla.

Imani ya Mamlaka kutoka kwa wadau imejengeka kutokana na mashirikiano makubwa ambayo wananchi wamekuwa wakiyaonesha tokea Mamlaka ilipoanza kazi rasmi mwaka 2015. Mashirikiano hayo yameifanya Mamlaka kupata mafanikio ya kupigiwa mfano.

Wakati Mamlaka inawashukuru sana wananchi wa Zanzibar kutokana na ushirikiano wao wanaoutoa, Mamlaka inazidi kuwaomba kutoa michango yao katika kuliendeleza Jarida hili la ZURA ambalo limeanzishwa ili kuwa daraja la kuwaunganisha wananchi wote katika kukuza huduma za maji na nishati kwa jumla.

Ustawi na maendeleo ya Jarida hili, vitategemea sana mawazo, fikra, maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau ambayo yatawasilishwa kupitia njia tofauti za mawasiliano kwa mtindo wa Makala, habari, picha na maoni kutoka sehemu mbali mbali za Zanzibar.

Michango itakayotolewa na wadau ni moja miongoni mwa njia zitakazotumiwa na Mamlaka kupata mrejesho na hivyo kuweza kujitathmini kutokana na huduma zinazotolewa na Mamlaka kwa jamii.

Madhumuni makubwa ya kuanzishwa Jarida hili ni kuwapatia wananchi taaluma na ufahamu juu ya majukumu ya Mamlaka na utekelezaji wake. Kinachotakiwa zaidi ni wananchi kufahamu vilivyo kazi za kila siku zinazofanywa na Mamlaka kwa ajili ya kuwahudumia wananchi ipasavyo.

Mamlaka imekabidhiwa jukumu la kudhibiti mambo muhimu ya maisha ya kila siku ya mwanadamu. Kutokana na kazi hiyo, Mamlaka inakuwa imesimama katikati baina ya watoa huduma na wanaotumia huduma hizo ambao ni wananchi.

Katika suala la udhibiti wa Huduma za Maji, Mamlaka inahakikisha kuwa maji yanayawafikia wananchi yakiwa katika hali ya ubora na usalama kwa maisha ya binadamu na viumbe hai. Aidha, Mamlaka inahakikisha kuwa watoa huduma za umeme, maji na gesi wanatoza bei ambazo wananchi wanazimudu kulingana na huduma zinazotolewa.

Kwa upande wa watoa huduma, Mamlaka itahakikisha kuwa nao wanapata faida stahiki kutokana na kazi wanayoifanya ili kuona kuwa utoaji wa huduma zao unakuwa endelevu.

Ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakuwa endelevu na kuwa na ubora unaokubalika, Mamlaka imeona ni vyema kuweko na mizania itakayosaidia kutambua udhaifu unaojitokeza mapema, kabla ya udhaifu huo kuanza kuleta athari katika sekta husika.

Matarajio ya Mamlaka ni kwamba Jarida la ZURA litasaidia katika kutanabahisha, kukosoa na kushauri njia sahihi zitakazoleta ufanisi zaidi na hatimaye kufikia malengo ya Mamlaka kwa maslahi ya taifa na wananchi wote kwa jumla.

Hivyo, Jarida la ZURA linaweza kutumika kama chombo shirikishi baina ya watoa huduma na watumiaji huduma na litatumika kama jukwaa la majadiliano baina ya Mamlaka na wadau kuhusiana na huduma za Maji, Umeme na Gesi Asilia.

# Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu ZURA



**Bw. Haji Kali Haji**
Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati, Zanzibar

**BODI** ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), inawashukuru sana wananchi wa Zanzibar kutokana na ushirikiano wa hali ya juu wanaoutoa kwa Mamlaka tangu kuanzishwa kwake.

Mamlaka ina muda mfupi tangu kuanzishwa kwake. Hata hivyo, ushirikiano ulioupata kutoka kwa wananchi wote wa Zanzibar umeifanya taasisi hii itekeleze majukumu yake vizuri na kwa ufanisi zaidi.

Kwa ajili ya kutimiza malengo yake kwa ufanisi, ZURA imeamua kuanzisha Jarida lake maalumu kwa lengo la kuwafikia kirahisi walengwa wake wakubwa ambao ni wananchi. Madhumuni ya kuanzishwa Jarida hili ni kuwapatia wananchi taaluma na ufahamu juu ya majukumu ya ZURA ili waweze kufahamu zaidi kazi za kila siku zinazofanywa na Mamlaka hiyo.

ZURA imeundwa kwa sheria nambari 7 ya mwaka 2013, iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ambapo jukumu lake kubwa ni kuhakikisha inadhibiti matumizi ya huduma za maji na nishati.

Katika udhibiti wa mambo hayo muhimu kwa maisha ya kila siku ya mwanadamu, ZURA inakuwepo katikati ili kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakuwa na ubora unaokubalika bila ya kumletea madhara mtumiaji.

Kwa mfano katika suala la udhibiti wa Huduma za Maji, ZURA ni lazima ihakikishe kuwa huduma ya maji inayotolewa kwa wananchi inawafika ikiwa katika hali ya ubora na usalama kwa maisha ya wananchi hao, binadamu wengine na viumbe wote hai.

Aidha, majukumu mengine ya Mamlaka hii ni kuhakikisha kuwa watoa huduma kama vile umeme, maji, gesi wanatoza bei ambazo wananchi wanazimudu kulingana na huduma zinazotolewa.

Kwa upande mwengine ZURA, inapaswa kuhakikisha watoa huduma hizo za maji, nishati ya umeme na gesi asilia nao wanapata faida katika utoaji wa huduma zao.

Katika kuhakikisha mambo hayo yanafanyika, ZURA imeunda kamati shirikishi baina ya watoa huduma na watumiaji huduma ambazo hukaa na kujadiliana suala la bei za huduma hizo hadi kufikia muafaka na hatimaye kuzitangaza kwa wananchi.

ZURA haishii kupanga bei tu, lakini huwa inafanya ukaguzi kwenye maeneo yanayotoa huduma, kupima na kuangalia ubora wa huduma kabla ya kuwafikia wananchi.

Kwa sababu Mamlaka inajukumu la kutoa leseni kwa wazalishaji, wasambazaji na wauzaji wa huduma za maji na nishati, wale wanaoshindwa kufikia viwango kwa mujibu wa sheria huwa wanawafutia leseni ama kuwafungia.

ZURA inajivunia ushirikiano inaoupata kutoka kwa wadau wote na wananchi kwa jumla na hilo ndilo linaloipa Mamlaka nguvu kutekeleza majukumu yake vyema.

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar napenda kuwahakikishia wananchi kwamba ni jukumu letu la kulinda maslahi ya wananchi tutalitekeleza kwa nguvu zetu zote.

Tunachowaomba wananchi na wadau wetu waendelee kushirikiana na ZURA na wasisite kufika ofisini kwetu pale linapojitokeza tatizo, na pia tunakaribisha maoni na ushauri wao.

KATIKA KUSIMAMIA HUDUMA BORA

# ZURA kuingia katika ushindani Duniani



Bodi ya wakurugenzi ya ZURA. Kutoka kulia waliokaa ni Mhe. Zakia Meghji, Mwenyekiti wa Bodi Bw. Mwalim Ali Mwalim na Mkurugenzi Mkuu wa ZURA, Bw. Haji Kali Haji. Waliosimama kutoka kushoto ni Bi. Bihindi Nassor Khatib, Bw. Ali Aboud Mzee, Bw. Salmin Sharif Khatib na Dk. Mohammed Dhamir Kombo.

**Na Khuzaimat Bakar**

**HISTORIA FUPI**

**TAASISI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati, Zanzibar (ZURA) imeasisiwa chini ya Kifungu namba 3 cha Sheria Namba 7 ya mwaka 2013, kwa kukabidhiwa kazi ya kudhibiti huduma za Maji na Nishati, Zanzibar. Sekta zinazodhibitiwa na Mamlaka hiyo ni pamoja na Mafuta, Gesi Nishati Asilia, Umeme na Maji.

Kuundwa kwa Mamlaka hii mwaka 2015, kumetokana na matakwa ya Sera ya Nishati ya Zanzibar ya mwaka 2009, ambayo imeeleza haja ya kuwepo mdhibiti anayejitegemea wa Sekta ya Nishati. Mageuzi hayo ya Sekta za Maji na Nishati yamo katika Mpango Mkuu wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA) pamoja na Dira ya 2020. Aidha, kuundwa kwa ZURA ni utekelezaji wa azma ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kutaka kuwepo taasisi za udhibiti wa sekta hizo kwa kila nchi mwanachama.

Kuanzishwa kwa ZURA ilikuwa ni kutimiza azma ya kudhibiti sekta za maji na nishati kwa dhamira ya kuhakikisha kuwa huduma hizo zinatolewa kwa ufanisi mkubwa. Lengo ni kuhakikisha kwamba watumiaji wanapata huduma zinazostahiki na wafanyabiashara wanapata faida halali kutokana na biashara zao ili kuleta faida za kiuchumi na kijamii (Economic and Socio Benefits).

**MAJUKUMU**

Kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha ZURA, kifungu cha 11 kinaainisha kazi na majukumu ya Mamlaka kama ifuatavyo:-

- Kuanzisha viwango vya bidhaa na huduma, zinazodhibitiwa; vigezo na masharti ya usambazaji bidhaa na huduma.

- Kuhakikisha kwamba watoa huduma wote wanatoa huduma bora na wanao mtaji wa kutosha kwa ajili ya kugharamia shughuli zao.
- Mamlaka inaweza kuandaa kanuni za maadili, matakwa ya kuripoti, muundo wa utumishi, kanuni za wafanyakazi na kitendo chochote kitakachokuwa muhimu kwa kudhibiti huduma hizo kwa ukamilifu;
- Kuwezesha na kushajiisha ushiriki wa sekta binafsi, ushindani mzuri, na kushiriki katika uwekezaji kwenye taasisi zinazotoa huduma;
- Kuhakikisha taasisi zinazotoa huduma zinatekeleza shughuli zao kwa mujibu wa Sheria;
- Kutunga Kanuni na kuweka miongozo kwa sekta zinazoshughulikia huduma;
- Kuanzisha na kutekeleza mfumo mzuri wa kuhakikisha kwamba wenye leseni wanatoa huduma kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na Kanuni na Sheria na kuzitangaza taarifa hizo kwa umma;
- Kuweka utaratibu wa kupokea, kuchunguza na kuyapatia ufumbuzi malalamiko ya wateja kuhusiana na huduma muhimu kwa muda utakaowekwa na kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii;
- Kuleta usuluhishi wa malalamiko na migogoro;
- Kutoa taarifa zinazohusu kazi zake;
- Kuzingatia kwa ukamilifu utunzaji na uhifadhi wa mazingira, uhifadhi wa vyanzo asilia, afya na usalama wa watumiaji;
- Kutoa maelekezo kwa watoa huduma wanaodhibitiwa.

Katika kutekeleza majukumu yake kikamilifu, Mamlaka imejipangia kazi zinazofanywa na ZURA katika kila sekta. Kazi hizo ni:

**Sekta ya Mafuta na Gesi**
- Kutoa, kufanya mapitio na kufuta sheria na kanuni za leseni zote zinahusiana na mafuta.
- Kudhibiti tozo kwa kushauriana na Waziri.
- Kushajiisha ushindani ulio bora kiuchumi.
- Kudhibiti viwango, ubora wa mafuta na gesi kwa kushirikiana na ZBS.
- Kusimamia miundombinu ya mafuta na Gesi ya serikali ikiwemo kuikodisha kwa watumiaji.

**Sekta ya Maji**
- Kudhibiti ubora na kiwango cha maji.
- Kupanga tozo, ushuru na gharama za maji kwa kushirikiana na Waziri.



Usambazaji wa Mabomba ya Maji eneo la Kianga kama inavyoonekana pichani ni sehemu ya juhudi za ZURA za kusimamia utoaji wa huduma bora za maji kwa wananchi.

- Kuhakikisha upatikanaji mzuri wa maji.
- Kutoa leseni za uendelezaji na usambazaji wa maji.

**Sekta ya Umeme**

- Kutoa, kufanya mapitio na kufuta leseni ya uzalishaji na usambazaji wa umeme.
- Kupanga tozo kwa kushirikiana na Waziri.
- Kudhibiti ubora na kiwango cha umeme.
- Kushajiisha ushindani ulio bora wa uzalishaji wa umeme.
- Kushiriki katika mikataba ya ununuaji umeme.

Katika kufanikisha kazi zake katika kila sekta, Mamlaka imejiwekea dira na dhamira maalumu zinazoongoza utekelezaji wa kila siku.

**Dira na Dhamira**

**Dira**

Dira kuu ya ZURA ni kuifanya taasisi hii kuwa miongoni mwa wadhibiti bora duniani wenye mfano wa kuigwa katika kusimamia utoaji wa huduma bora za Maji na Nishati.

**Dhamira**

Dhamira ya mamlaka ni kusimamia huduma za Nishati na Maji kwa uwazi na ufanisi ili kukuza uwekezaji na kuchangia maendeleo ya kiuchumi Zanzibar.



Pichani ni ziara ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakiangalia mradi wa ujenzi wa Tangi la Maji Saateni. Ziara hiyo ni sehemu ya kutekeleza dhamira ya ZURA ya kutoa huduma kwa uwazi na ufanisi.

# Maji humimina viini vya uhai



Ofisa wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) akipima kiwango cha ubora wa maji chini ya uangalizi wa maofisa wa ZURA kutoka kushoto Bi. Zeyana Ali Mwalimu, Bw. Khamis Ali Khamis na Bi. Latifa Amour Zaid.

**Na Mbarak Hassan**

**MAJI** ni uhai, ni tamko linalomaanisha kwamba kitu chochote kilichohai ni lazima kitegemee kuwepo kwa maji. Maji ni neema inayotoka kwa Mola Muumba.

Wanasayansi wanaeleza kuwa maji yanatokana na molekuli (molecule) yenye atomi (atoms) mbili za haidrojeni na atomi moja ya oksijin ($H_20$) Molekuli hizo ndizo zinazounda kitu kiitwacho maji.

Maji hutumika kwa matumizi mbali mbali. Hakuna kinywaji muhimu duniani zaidi ya maji. Lakini kunywa maji safi na salama ni jambo linalohitajika kwa kila mtu. Maji hupatikana toka katika chemchem, mvua na vyanzo vingine vingi kama vile maji madini ya visima virefu.

Umuhimu wa maji kwa binadamu ni mkubwa kiasi kwamba wataalamu wa afya wa aina zote duniani wamekiri kuwa maji ni kiendelezo cha uhai.

Binadamu huyatumia maji kwa ajili ya kunywa, kuoga, kupikia, kuoshea na shughuli nyingine nyingi, lakini pia huyatumia kwa shughuli za kiroho kama kujitoharisha, kubatiza, kusilimisha, kutibu, kuapisha na kadhalika.

Kila mtu anajua umuhimu wa maji katika shughuli zake za maisha. Takwimu zinaonesha kuwa mwili wa mwanadamu umejengwa kwa maji kwa zaidi ya asilimia 70.

Mbali na hayo, mwili pia unahitajia maji kwa kiasi kikubwa ili kufanya kazi zake vyema. Je, unajua kwamba mapafu yako yanahitajia vikombe viwili (2) vya maji hadi vinne (4) kila siku ili kufanikisha kazi yake ya kupumua? Kiasi hicho huhitajika zaidi wakati wa baridi.

Wakati binadamu apotoka jasho, kikombe kimoja cha maji hupungua mwilini mwake. Mtu anapokoga wakati wa mchana ikiwa ni mara ya tatu kwa siku inakuwa ni kama amekunywa vikombe sita (6) vya maji.

Kunywa maji ya kutosha husaidia kupunguza uwezekano wa kutokea mawe katika figo, hulainisha viungo na kuzuia mafua pia kusaidia kupona haraka ugonjwa huo.



Maofisa wa ZURA wakikagua hali ya mabomba ya maji katika Mkoa wa Kaskazini Pemba ili kuhakikisha maji yanayowafikia wananchi ni safi na salama

Maji ni mahitajio ya dharura kwa afya za binadamu, kwani asilimia 60 ya uzito wa binaadamu ni maji na mfumo wa mwili wake hutegemea maji ili kufanya kazi zake.

Ukosefu wa maji mwilini humfanya mtu akaukiwe na maji (dehydration), hali ambayo hutokea pale mtu anapokosa maji ya kutosha mwilini ya kuuwezesha mwili wake kufanya kazi zake za kawaida. Hata unapotokea upungufu mdogo wa maji mwilini, inakadiriwa asilimia moja (1%) hadi mbili (2%) ya uzito wa mwili unapungua. Suala hilo humfanya mtu akose nguvu na kujisika amechoka.

Hapa linajitokeza swali, ni zipi dalili za upungufu wa maji mwilini? Miongoni mwa dalili za upungufu wa maji mwilini ni mtu kuhisi kiu sana, uchovu, kuumwa na kichwa, mdomo kukauka, kutopata haja ndogo kwa muda mrefu au kupata haja ndogo kwa kiwango kidogo. Dalili nyingine ni udhaifu wa misuli na kuhisi kizunguzungu.

Kunywa maji safi na salama kwa kiasi kinachostahiki kiafya kunaweza kuboresha maisha na kumfanya mtu ajihisi mwenye afya na furaha zaidi. Kunywa maji ya kutosha kuna faida nyingi. Zifuatazo ni baadhi ya faida unazopata mwili kutokana na kunywa maji ya kutosha.

Kwanza, maji husaidia mmeng'enyo wa chakula. Vimeng'enya na kemikali mbalimbali zinazohusika na mmen'genyo au usagaji wa chakula mwilini ziko katika hali ya mchanganyiko na maji na ili viweze kufanya kazi vizuri inatakiwa kuwe na uiano sahihi kati yake na maji.

Pili, maji yanahusika katika kulainisha baadhi ya vyakula. Kunywa maji ya kutosha kunaongeza ufanisi wa mwili katika kulainisha chakula. Wataalamu wanasema kuwa maji huimarisha afya ya ngozi. Kunywa maji ya kutosha hung'arisha ngozi na kuipa muonekano mzuri na husaidia tishu za ngozi kuwa bora na kuongeza unyevu kwenye ngozi.

Tatu, maji husaidia katika utendaji kazi wa ubongo. Maji yanauweka ubongo katika hali nzuri zaidi na kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Kunywa maji ya kutosha kunamwezesha mtu kuwa na uwezo mkubwa wa kufikiri. Faida nyingine za maji ni kupunguza uwezekano wa kupata baadhi ya magonjwa hatari ya mafua, mawe ya figo, matatizo ya ini, baadhi ya saratani na magonjwa mengine.

Aidha, faida nyingine ya maji ni kutatua na kuzuia tatizo la kukaukiwa na haja kubwa (constipation). Kunywa maji ya kutosha kunaweza kusaidia kupata haja kubwa kiulaini na pia kumuepusha mtu na choo kigumu.

Maji ya kutosha yanasaidia kupunguza tatizo la kubanwa misuli na pia hupunguza msuguano katika viungo. Aidha, huondoa uchovu, huchochea shughuli za kimetaboliki mwilini pamoja na kusaidia katika suala zima la kupunguza uzito. Hivyo, kama mtu yuko katika mkakati wa kupunguza uzito, maji yanaweza kumsaidia kwa kiasi kikubwa.

Maji huongeza kasi ya shughuli za kimetaboliki mwilini. Ongezeko hilo la kimetaboliki husababisha mwili kutumia nishati nyingi zaidi na hivyo huweza kupunguza kiasi cha nishati ambacho kitahifadhiwa mwilini katika hali ya mafuta. Ongezeko la ufanisi wa figo na ini kutokana na kunywa maji ya kutosha husaidia kuondoa mafuta ya ziada mwilini.

# Wauza gesi kupatiwa leseni



Wajumbe wa Bodi ya ZURA wakiangalia mitambo inayoweka gesi kwenye mitungi iliyoko Manga Pwani Zanzibar

**Na Hassan Amour**

KWA kiwango cha wastani wananchi wa Zanzibar wameanza kutumia gesi kwa shughuli zao za nyumbani hasa kupikia.

Hayo ni mafanikio makubwa kwani gesi inaweza kuwa njia mbadala ya kuinusuru nchi kugeuka kuwa jangwa kutokana na miti kuteketea kwa kukatwa kwa ajili ya upatikanaji wa kuni na makaa ya kupikia.

Tafiti mbalimbali zinazoendelea kufanywa ulimwenguni zinabainisha kasi kubwa ya upoteaji wa misitu hali inayopelekea kuwepo kwa ongezeko la joto, ambalo chanzo chake ni uzalishaji wa gesi zinazochafua hali ya hewa.

Zanzibar kama sehemu ya ulimwengu nayo imekuwa ikikabiliwa na matokeo hasi ya ongezeko la joto duniani ambayo yamebatizwa jina maarufu kwa kuitwa athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Katika visiwa vyote vya Unguja na Pemba, athari za tabia nchi zinaonekana wazi, kwani yapo baadhi ya maeneo yalioyokuwa yakitumika kwa kilimo ambayo wakulima wameyahama kutokana na kuvamiwa na maji ya chumvi.

Kwa mujibu wa Idara ya Mazingira Zanzibar maeneo ambayo maji ya chumvi yamevamia ni Charawe, Makunduchi, Tumbe, Mkoani, Micheweni, Msuka na Wesha.

Aidha, watafiti wa masuala ya hali ya hewa, wanaeleza wazi kuwa athari za tabia nchi kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikichangiwa na ukataji ovyo wa misitu.

Hoja ya wataalamu hao ni kwamba uzagaaji wa gesi chafu zinazozalishwa hasa kutoka viwandani, ungeweza kudhibitiwa kwa upandaji miti ambayo inavuta hewa ya kabonidaiokside ($CO_2$).

Zanzibar imekuwa ikipoteza mamia ya hekta za misitu inayokatwa na kutumiwa na



Maofisa wa ZURA wakiwa kwenye kikao na wadau gesi. Kikao hicho ni cha kujadili utaratibu utakaotumika katika utoaji wa leseni kwa wafanyabiashara ya gesi ya kupikia.

wananchi kwa shughuli zao mbalimbali za kimaendeleo. Hata hivyo, sehemu kubwa ya misitu inayokatwa hutumika kwa uzalishaji wa nishati kama kuni za kupikia na kufanywa makaa kwa ajili ya uzalishaji wa nishati ya kupikia.

Ni wazi jamii ikiendelea kutumia misitu kama chanzo cha nishati ya kupikia kwa ajili ya kuni na makaa, ipo siku Zanzibar itakuwa jangwa na zile athari za tabia nchi zitaitafuna nchi kama si kuimeza kabisa.

Zipo njia nyingi za kuhifadhi misitu isifanywe kama chanzo cha kuzalisha nishati ya kupikia kama kuni na makaa. Njia hizo ni pamoja na watu kupikia kwa kutumia nishati ya umeme na matumizi ya gesi.

Tunaelewa suala la mwananchi wa kawaida kutumia umeme kwa ajili ya nishati ya kupikia ni gumu kutokana na uwezo wa kumudu gharama za umeme.

Hata hivyo, hivi sasa matumizi ya gesi (Liquefied Petroleum Gas - LPG) kwa ajili ya kupikia yameanza kuingia kwa kasi Zanzibar. Watu wengi kutokana na kuhamasika wameanza kutumia gesi kwa ajili ya shughuli zao za mapishi.

Gesi imeanza kuingia sokoni na kuwa biashara muhimu ambapo kampuni mbali mbali hivi sasa zinauza bidhaa hiyo kwa wananchi. Katika kulifahamu hilo, serikali nayo imelazimika kuliwekea utaratibu maalumu.

Kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), bidhaa ya gesi imewekewa utaratibu wa jinsi itakavyotumika na namna itakavyoendeshwa.

ZURA inaeleza kuwa, moja kati ya majukumu yake ni kuhakikisha kuwa bidhaa ya gesi kabla ya kumfikia mwananchi kwa ajili ya matumizi, inakuwa kwenye kiwango kizuri na salama.

Aidha, jukumu jengine la ZURA katika kuisimamia nishati hiyo ni kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza kuimudu bei inayouzwa bidhaa hiyo.

Sambamba na hilo, kampuni zenye kuuza gesi kwa ajili ya matumizi ya nishati ya kupikia nazo zinafanya biashara hiyo kwa faida.

ZURA iko katika hatua za mwisho za kuanza kuzipatia leseni kampuni zenye kuingiza nishati ya gesi visiwani hapa. Kilichochelewesha ni kumalizika kwa muongozo na kanuni ambazo zinawataka wenye kampuni kubwa na ndogo zenye kutoa huduma ya gesi kukata leseni maalumu.

Hata hivyo, ZURA inawaomba wananchi kuchukua tahadhari zaidi kwenye matumizi ya gesi, ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi yasiojali miongozo ya kiusalama kwenye utumiaji wa gesi.

# ZURA Kudhibiti upandaji holela bei ya umeme



Ofisa wa Usalama na Mazingira Bi. Latifa Amour Zaid akimuhoji Ofisa wa Shirika la Umeme Zanzibar (mwenye shati jeupe) kuhusu uhakika wa utoaji wa huduma ya umeme katika mitambo ya utoaji wa umeme iliyoko Mwanyanya Wilaya ya Magharibi A, Unguja.

**Na Khuzaimat Bakar**

KILIO cha upandaji wa bei ya nishati ya umeme bila ya kuzingatia hali ya wateja ni hali iliyokuwepo kwa muda mrefu na kwamba wananchi wengi wamekuwa wakiilalamikia hali hiyo licha ya kuwa kila kukicha idadi ya wanaopatiwa huduma hiyo imekuwa ikiongezeka.

Ni wazi tabia ya kupanda kiholela bei ya umeme inakera. Hali ya kuendelea kuongezeka idadi ya wananchi wanaohitaji kuunganishwa kwenye huduma hiyo isichukuliwe kwamba watu hawaudhiki na tabia hiyo. Sababu hasa ya kuongezeka kwa wateja inatokana na ulazima uliopo wa watu kutumia nishati ya umeme kwa ajili ya maendeleo yao ya kila siku.

Inakuwa vigumu kufikiria inakuwaje kama inatokea siku moja watu wanaamka hakuna nishati ya umeme, halafu hapo hapo zinatolewa taarifa za kitaalamu kuwa duniani hakutakuwa na huduma hiyo tena.

Bila ya shaka maisha yataendelea duniani kwa kukosa umeme, lakini yatawafanya wanaadamu kuwa kwenye dhiki kubwa kwani kila kitu kitafanyika taratibu na shughuli nyengine kutokufanyika kabisa. Kwa maana nyengine ni kurejea kuishi maisha ya enzi za mawe.

Kutokuwepo umeme duniani, maana yake ni kwamba hakutakuwa na mashine wala mitambo yoyote ambayo hivi leo inatumika kwenye uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma.

Aidha, kitu kinachoitwa mawasiliano nayo huyatakuwepo kwa sababu ili mtu asikilize redio, atizame televisheni na asome gazeti akiwa nyumbani, umeme lazima utumike kabla ya kupata huduma hizo.

Mawasiliano ya simu za mkononi ambayo leo yamerahisisha sana maisha ya wanaadamu, nayo hayatakuwepo. Hivyo ule utamaduni wa zamani utarejea ambapo endapo mtu amepata msiba atalazimika kufunga safari masafa marefu kwa ajili ya kwenda kutoa taarifa kwa sababu simu, redio na televisheni zitakuwa hazipo tena.




Pichani ni kikao cha pamoja kati ya watendaji wa ZURA, ZECO na wadau wengine. Kikao hicho ni kwa ajili ya kuangalia gharama za uendeshaji wa umeme ili kupanga bei ya umeme kwa wananchi.

Kutokana na nadharia hii, inaonesha dhahiri mwanadamu yeyote hivi leo maisha yake yamekuwa tegemezi dhidi ya nishati ya umeme.

Maisha yamekuwa tegemezi kwa sababu uvumbuzi wa nishati ya umeme umerahisisha kila kitu na ni chanzo cha kufikia mafanikio ya kiuchumi na kijamii kwa kasi kubwa.

Hapana wasiwasi maisha ya binadamu yamebadilika sana. Katika kipindi kidogo kilichopita, huduma ya umeme Zanzibar ilikuwa ni kwa watu wenye uwezo mkubwa pekee. Ilizoeleka kwamba nyumba yenye umeme ilikuwa ni nyumba ya tajiri au ya mtu mwenye kujiweza.

Kihistoria, wananchi wengi walikuwa wakiichukulia nishati ya umeme kama anasa na sio huduma za kurahisisha maisha ya kila siku ya mwananchi.

Maisha Zanzibar hivi sasa yamebadilika sana. Kampeni mbalimbali zilizofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimesaidia sana watu kutambua umuhimu wa umeme.

Hivi sasa matumizi ya nishati ya umeme katika nyumba sio anasa tena, bali ni huduma muhimu ya kuchapuza na kuharakisha maisha ya kila mwana familia.

Nyumba hata inayojengwa kijijini, miongoni mwa mipango muhimu baada ya kukamilika ni kuunganishwa huduma ya umeme kwa matumizi ya nishati kwa ajili ya taa za kuonea, kupikia na kusaidia kuendesha mashine ndogo ndogo kama mafriji, mafeni na kadhalika.

Kutokana na mwamko na kasi ya matumizi ya nishati ya umeme, Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) ambalo ndilo lenye jukumu la kusambaza umeme pia lilikuwa likipanga bei ya nishati hiyo pengine bila kuzingatia sana hali za wateja.

Kilio hiki kimekuwepo muda mrefu, lakini hatimaye Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekipatia ufumbuzi kwa kuunda Mamlaka maalumu ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), ambayo moja ya jukumu kubwa la Mamlaka hii ni kuhakikisha inaangalia utoaji wa huduma za uhakika na zenye kumuwezesha mwananchi wa kawaida kumudu kuzilipia.

Mipango iliyokuwepo ni kwamba ZURA itaanza rasmi kutoa leseni kwa Mashirika, Kampuni ama Taasisi ambazo hujishughulisha na uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati ya umeme. Kwa msingi huo, ili Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) liweze kutekeleza vyema majukumu yake lazima lipate leseni ya huduma inazozitoa kutoka kwa ZURA.

Chini ya utaratibu wa utoaji leseni, kwa mfano mtu ana jenereta lenye uwezo wa 1000 KVA ambalo analitumia kuwaunganisha wengine kwa malipo, naye atalazimika kukata leseni.

Majukumu haya yote yatatekelezwa na kusimamiwa chini ya kamati maalumu itakayoundwa ambayo itakuwa na jukumu la kuangalia haki za mteja na haki za mtoa huduma.

Kuhusu kilio cha muda mrefu cha Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kuwapangia bei ya umeme wananchi, suala hilo hivi sasa halitakuwepo tena.

ZECO wakitaka kubadilisha bei ya umeme watalazimika kupeleka maombi yao ZURA ambayo itaangalia mambo kadhaa ikiwemo ridhaa ya wananchi kabla ya kuridhia ama kutoridhia kwa ombi hilo la ZECO.

# Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)



Ewe Mwananchi kwa matatizo yote ya umeme kama vile nguzo mbovu, kukosa umeme, mita yako kutokufanya kazi au kuharibika, kuchelewa kupatiwa huduma ya kupimiwa na matatizo mengine yanayohusu huduma zetu hakikisha unawasilisha matatizo yako ZECO wakati wowote ndani ya saa 24 kwa kupiga simu 0772877879 au 0242230232 utasikilizwa na kuhudumiwa bila ya wewe kufika katika ofisi zetu. Toa taarifa sahihi ili uhudumiwe kwa haraka.

ZECO tupo kung'arisha maisha yako

# Adha ya kuadimika Mafuta imeondoka

**Na Mbarak Hassan**

**TOKEA** kuanzishwa kwake mwaka 2015, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) imeweza kuleta uimara wa soko la bidhaa za mafuta ikiwemo petroli, dizeli na mafuta ya taa hapa Zanzibar.

Kabla ya kuanzishwa kwa ZURA soko la bidhaa za mafuta ya petroli halikuwa la uhakika sana visiwani na zaidi kulikuwa na ukosefu wa mara kwa mara wa mafuta Zanzibar hali iliyosababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi.

Uhaba pekee unaoonekana kutokea hivi sasa ni ule unaosababishwa na kuingizwa mafuta yasiyokidhi kiwango ambapo hulazimika kurejeshwa yalikotoka na kwa kuwa kumekuwa na uhaba wa matangi ya kuhifadhia mafuta, ndio hutokea kukosekana kwa mafuta kwa muda mchache.

Zanzibar ilikuwa ikiingia katika kipindi cha taharika na mitihani ya shida ya kuadimika kwa mafuta ya petroli na dizeli na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi, hasa wafanyakazi na wafanyabiashara wanaofanikisha kazi zao kwa kuwepo kwa usafiri wa uhakika.

Ukosefu wa mafuta ya dizeli na petroli kwa kila wakati Zanzibar ilikuwa na changamoto kubwa sana; shughuli nyingi za maendeleo ziliweza kusimama ama kukwama, wananchi walikuwa na wakati mgumu na wakati mwengine kuweza kusumbuka kwa muda mrefu kuweza kufanikisha upatikanaji wa bidhaa hiyo.

Biashara ya mafuta machafu iliingia mtaani, wakati mwengine kushuhudia gari zikishindwa kufanyakazi kutokana na uchakachuaji wa mafuta uliofanyika. Kiwango kikubwa cha mafuta ya petroli na diseli kikiwa kimechanganywa na mafuta ya taa ama wakati mwengine kushuhudia kiwango kikubwa cha mafuta kikiwa kimechanganywa na maji.

Ubora wa mafuta haukuwepo Zanzibar hali iliyotoa mashaka makubwa kwa watumiaji kupoteza imani ya kiwango cha matumizi cha bidhaa hiyo muhimu kutokana na wajanja wachache kwa upande mwengine wakiongeza kasi ya kujinufaisha kutokana na mahitaji ya wengine.

Kuanzishwa kwa ZURA, kulitia hofu kubwa kwa wafanya biashara wa bidhaa ya mafuta Zanzibar wengi wakidhani kwamba biashara ya mafuta visiwani sasa imedhibitiwa, bei itakuwa ikipangwa na ZURA bila ya kuangalia faida au mapato makubwa ya wafanyabiashara hao.

Hofu hiyo ilipelekea kwa wafanyabiashara wengi wa mafuta Zanzibar kutaka kusitisha kuagiza mafuta wakidhani kwamba Zanzibar sasa hakuna haja ya kuendesha biashara hiyo kwa kuwa udhibiti mkubwa utakaofanyika utalenga zaidi kwa waagizaji kuliko kwa watumizi.

Katika hili, ZURA iliwahakikishia wafanyabiashara kuwa biashara wanayoendesha ya bidhaa za mafuta ya petroli na diseli wanapata faida stahiki na wananchi hawatozwi bei isiyostahiki.

Kwa hatua hiyo, ZURA wameweza kuweka utaratibu ambao unamuhakikishia mfanyabiashara na mteja kuwa wanapata bei inayostahiki kwa mujibu wa bei halisi za bidhaa hiyo katika soko la dunia.

Utata unaondoka, biashara inakuwa wazi kwa wafanyabiashra kuwa na uhakika na wanachokipata. Uwazi unakuwepo wa kinachoingizwa na kinachunguzwa ubora wake. Wafanyabiashara hawataligomea soko la mafuta ama kuficha bidhaa hiyo.

Katika kipindi cha miaka miwili tokea kuanzishwa ZURA tumeshuhudia kuondoka ile tabia ya wafanyabiashara kuficha bidhaa hiyo na kusubiri kuadimika katika vituo vyote vya mafuta ili wajitokeze wakiwa tayari wameshapandisha bei wanayoitaka wao.




Watendaji wa ZURA wakikagua mashine kutilia mafuta kwa lengo la kuthibitisha kiwango cha mafuta kinachopitisha mashine hiyo ni sawa na fedha zinazotolewa na wateja.

Hili lilikuwa jambo la kawaida kwa Zanzibar, ushahidi ni kuwepo kwa misururu mirefu ya wananchi kusubiri mafuta katika vituo mbali mbali. Kazi na shughuli zikisimama kutokana na sababu ya kuadimika kwa mafuta visiwani.

Kwa Zanzibar matukio ya kuadimika mafuta kwa kisingizio cha kufichwa na wafanyabiashara wa bidhaa hiyo sasa hakipo tena. ZURA imefanikisha kwa kuweka uwazi kabisa bei ya bidhaa hiyo katika soko la ndani kufuatia upatikanaji wake katika soko la dunia.

Kwa mnasaba huo, ZURA sasa ina 'meno'. Imekuwa ikiangalia na kudhibiti mwenendo mzima wa biashara ya mafuta Zanzibar. Wajanja na wapiga 'dili' wa bidhaa hiyo sasa hawana cha kufanya. Taratibu za kisheria zinafuatwa katika kuhakikisha kuwa mafuta yanakuwepo Zanzibar yakiwa na kiwango cha uhakika kwa ajili ya matumizi.

Katika kuhakikisha kuwa ZURA inakuwa chombo imara, chenye kutegemewa kati ya wafanyabiashara na watumizi hasa katika kufikia kiwango cha kimataifa kama zilivyo katika nchi nyengine nyingi ambazo zimeandaa mamlaka inayofanana na ZURA, imeandaa kanuni mbali mbali ambazo sasa zimo katika hatua ya ukamilishwaji.

Upatikanaji na ukamilishaji wa kanuni hizo utaifanya ZURA kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa na azma ya uimara wa chombo hicho utajitokeza kutokana na usimamizi na ufuatiliaji.

Miongoni mwa kanuni hizo ni pamoja na Kanuni za Usimamizi wa Vituo vya Mafuta (The Petroleum Filling Stations Regulations), Kanuni za Usimamizi wa Biashara ya Mafuta (Petroleum Supply Regulations) na Kanuni za Uagizaji Mafuta wa Pamoja (Petroleum Bulk Procurement Regulations).

# Zanzibar Water Authority (ZAWA)

Let's sustain our clean and safe water
Pay today to see its sustainability.

## Our offices are everywhere to serve our customers

Urban - Madema
Nouth 'A' - Gamba
North 'B' - Mahonda
West 'B' - Kijitoupele
Wete Pemba - Taifu

West "A" - Mwera
Centre Unguja - Koani
South Unguja - Paje
Pemba Chake - Machomane
Mkoani Pemba - Uweleni
Micheweni Pemba - Kilindi

For more information
Contact us:
0774 777 777

# ZURA na changamoto zake




**Na Hassan Amour**

**KAMA** ilivyo kwenye taasisi nyengine nyingi, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) nayo imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbali mbali kadri shughuli za mamlaka hiyo zinavyozidi kushika kasi.

Jitihada za kukabiliana na changamoto hizo ndizo zinazoipa kasi zaidi ZURA katika kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake ya udhibiti wa huduma za maji na nishati na hasa katika sekta ya mafuta ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikilalamikiwa kutokana na kukosekana ufanisi katika baadhi ya mambo.

Katika kuona changamoto hiyo inapatiwa ufumbuzi wa kudumu, ZURA hufanya ukaguzi wa mara kwa mara kuhakikisha kuwa bidhaa ya mafuta inakuwa katika kiwango stahili na wananchi wanaitumia bidhaa hiyo ikiwa katika hali ya bora na kiwango kinachokubalika.

Sambamba na hatua hiyo, mfumo wa utoaji leseni kwa vituo vya mafuta ni miongoni mwa mikakati ya ZURA kuhakikisha kwamba vituo hivyo vinaendesha shughuli zake kwa ufanisi mkubwa.

Maamuzi ya hatua hizo yanatokana na ukweli kwamba haitoshi pekee kusema kwamba Zanzibar imeanzisha mfumo wa leseni kwa vituo vya mafuta bila ya kuusimamia mfumo wenyewe na kuhakikisha kuwa malengo ya kuanzishwa kwake yanafikiwa.

Nchi kadhaa zikiwemo za Kusini mwa Jangwa la Sahara zilizoamua kuweka ubora katika biashara ya

Magendo ya mafuta ni miongoni mwa changamoto zinazoikabili ZURA. Askari polisi wa Kituo cha Unguja Ukuu Wilaya ya Kati wamezikamata chupa zenye mafuta ya Petroli zikiwa zimehifadhiwa kwenye nyumba zikisubiri kuuzwa kwa magendo.



Uhifadhi ya mafuta ya magendo uliogunduliwa huko Unguja Ukuu ambapo muhusika akihifadhi madumu ya Petroli kwenye hodhi lililo ndani ya nyumba yake.

mafuta kwa lengo la kumpatia faida muuzaji na mtumiaji, zimeanzisha mfumo wa leseni katika biashara hiyo.

Linalifaa kujiuliza, ni kweli vituo vya mafuta Zanzibar vinakidhi kiwango; na kiwango kipi kinachohitajiwa na ZURA? Haya ni miongoni mwa masuala ya msingi ambayo wananchi wengi pamoja na wafanyabiashara wa mafuta wamekuwa wakijiuliza kwa muda mrefu kabla ya kuanzishwa kwa mfumo huo visiwani.

Kitaalamu vituo vya mafuta lazima viwe na viwango ambavyo vinatambulika kimataifa. Viwango hivyo pamoja na mambo mengine vina lengo la kuhakikisha usalama wa vituo vya mafuta.

Ithibati ya hili ni kwamba sio mahali popote panaweza kujengwa kituo cha mafuta. Vituo vya mafuta vinapaswa kujengwa ama kuanzishwa mahali maalumu kwa lengo la kuhakikisha kwamba eneo hilo haliwezi kuwa sehemu inayoweza kusababisha madhara kwa binaadamu kutokana na biashara inayokusudiwa kufanywa.

Mara kadhaa ulimwenguni yameshuhudiwa maafa makubwa yakitokea kutokana na miripuko ya vituo vya mafuta. Kwa hapa Zanzibar maafa yameshuhudiwa katika vituo "bubu" vya mafuta. Miripuko mingi kati ya hiyo imesababisha vifo au kuchangia kuongezeka kwa idadi ya maafa katika sehemu yanapotokezea maafa hayo.

Kituo cha mafuta kuwa karibu sana na nyumba za makaazi ya binaadamu, kinakuwa ni chanzo cha maafa wakati madhara ya mripuko yanapotokea katika kituo hicho cha mafuta.

ZURA imeliona hili, ndio maana ikahakikisha kunakuwepo ukaguzi katika vituo vya mafuta ili kuweza kujiridhisha na usalama wa maeneo hayo kwa lengo la kuepuka majanga makubwa yanayoweza kutokezea hadi kupelekea kuwa majanga ya kitaifa.

Miongoni mwa miongozo ya ZURA katika kufanikisha hili ni kuweka na kutambua masafa maalumu baina ya kituo kimoja cha kuuzia mafuta hadi kingine. Muongozo huu ni kujaribu kuzuia kuongezeka kwa utitiri wa vituo vya kuuziwa mafuta Zanzibar.

Sio vibaya wananchi wengi kuhamasika katika uendelezaji wa biashara hiyo ya mafuta, pengine kutokana na faida inayopatikana, lakini taratibu za kisheria na kiusalama za uendeshaji wake zinapaswa kudhibitiwa.

Katika hili, muongozo unataka uwepo wa kituo kimoja cha mafuta hadi kingine ni kilomita moja (1). Muongozo huu pia unapambanua uwazi wa uendeshaji wa biashara ya mafuta kwani mwenye nia ya kufanya biashara atawajibika kuchagua eneo linalokubalika la kuendesha biashara yake na sio katika eneo lolote analotaka.

Eneo jengine linaloangaliwa ni usalama wa uwepo wa vituo vya kuuzia mafuta. Tahadhari kubwa zinachukuliwa za kuhakikisha usalama katika maeneo ya vituo unakuwepo ikiwa ni pamoja na haja ya kukinga ajali ambazo zinaweza

kuwa chanzo kikubwa kinachoweza kusababisha miripuko.

Ajali zinazosababishwa na mafuta zinapotokea hazisababishi tu miripuko lakini pia zinahusisha ajali nyengine za kawaida kutokana na uasili wake. Ni chanzo kinachosababisha kupoteza maisha na uharibifu mkubwa wa mali za watu wengine waliokaribu na tukio hilo.

Hii ndio changamoto kubwa kwa ZURA iliyokuja na wazo la kutaka kituo cha kuuzia mafuta kisiwe na aina zozote zinazoweza kusababisha maafa mengine pale unapotokea mripuko.

Katika kituo salama cha kuuzia mafuta kinatakiwa pamoja na mambo mengine kisiwe karibu na kona ama barabara ya muunganisho (junction). ZURA inataja kituo cha kuuzia mafuta kiwepo katika eneo tambarare na lililonyooka ili kuweza kupunguza kasi ya ajali au kudhibiti ajali inapotokea.

ZURA katika kuhakikisha kwamba udhibiti na ubora wa mafuta unapatikana kwa kiwango, hivi karibuni inatarajia kuanzisha maabara maalum ya upimaji wa mafuta kabla ya kuanza kutumika. Hatua hii ya ZURA itapambanua ni mfanyabiashara yupi anayeharibu biashara ya mafuta nchini kwa kuingiza bidhaa iliyo chini ya kiwango.

Aidha, hatua hii itaiwezesha ZURA kupita katika kituo kimoja kimoja kuangalia uhalali na uhalisia wa bidhaa ya mafuta katika vituo iwapo inakidhi kiwango. Lengo ni kumlinda mteja ili asiathirike na bidhaa iliyochakachuliwa.

Suala la upimaji wa mafuta litaweza kutumika kama 'tiba' ya waendesha biashara ya magendo ya mafuta pamoja na uwepo wa vituo holela na visivyosajiliwa vya mafuta nchini. Katika kufanikisha hili, ZURA pamoja na mambo mengine itaweza kusimamisha vyombo na kupima ubora wa mafuta yanayotumika.

Athari ya kuwepo vituo holela vya kuuzia mafuta imekuwa ikizungumzwa kwa muda mrefu ambapo pamoja na mambo mengi uibukaji wa vituo hivi umekuwa ukiikosesha serikali mapato na pia kuharibu ubora wa mafuta yanayoingizwa nchini na kutumiwa na wananchi.




Kituo cha mafuta cha Chake Chake Pemba (Kabla ya kufanyiwa matengenezo) ambapo kilikuwa kinatoa taswira ya kukosa ubora wa vituo vinavyohitajika kutokana ujenzi wake kutokukidhi vigezo




Ofisa wa Kitengo cha Uhusiano wa ZURA Bi. Kuzaimat akitangaza bei ya mafuta ya mwezi kwenye jengo la Makao Makuu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar

# UFAHAMU MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA ZANZIBAR

**Na Mbarak Hassan**

**KUTOKANA** na watu wengi kutofahamu jinsi bei ya mafuta zivyopangwa, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) imetoa ufafanuzi juu ya hali halisi kuhusiana na upangaji wa bei za mafuta nchini kulingana na bei za mafuta katika soko la Dunia.

Hatua hiyo inatokana na malalamiko ya muda mrefu kwamba bei za mafuta Zanzibar hazishuki wakati ambapo bei katika soko la dunia zimekuwa zikishuka kila siku, dhana ambayo ZURA imeeleza kuwa sio sahihi.

Tokea Februari, 2016 Mamlaka ilipoanza rasmi kupanga bei za bidhaa za mafuta, baada ya kukabidhiwa majukumu hayo na Bodi ya Mapato Zanzibar, ZURA imekuwa ikitangaza bei za mafuta kila mwezi kwa kuzingatia gharama halisi.

Mamlaka kila mwezi inapanga na kutangaza bei za bidhaa za mafuta ili kuhakikisha kwamba bidhaa za mafuta zinapatikana bila usumbufu na kwa bei halali kwa kuzingatia gharama halisi.

Utaratibu unaotumika kwa Zanzibar ni kuwa mafuta yanaagizwa na kuingizwa nchini kupitia kampuni nne zilizosajiliwa ambazo ni United Petroleumm (UP), GAPCO, Zanzibar Petroleum (ZP) na PUMA.

Kampuni hizo huwa hazinunui

mafuta na kuyaleta Zanzibar moja kwa moja kutoka katika soko la dunia, bali huyanunua kupitia mfumo wa ununuaji wa pamoja wa mafuta Tanzania Bara (BPS) au kutoka Kenya kupitia mfumo uliowazi wa zabuni ''Open Tender System'' (OTS).

Baada ya kuwasili katika Bandari ya Dar es Salaam, mafuta hayo husafirishwa na kuletwa Zanzibar, kutokana na unafuu wa uagiziaji wa mafuta kupitia mfumo huo wa uagiziaji wa pamoja.

Mamlaka inapanga bei kwa kuzingatia bei halisi na gharama zinazohusiana na uagiziaji, uhifadhi na usafirishaji wa mafuta hadi Zanzibar.

Kuna vigezo tisa (9) vinavyotumiwa na ZURA katika kupanga bei ya mafuta, ambavyo ni:

- **Moja,** wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani (platts quotations) kwa mwezi husika wa uagizaji mafuta hayo.
- **Pili,** gharama halisi za usafirishaji hadi katika Bandari ya Dar es Salaam, Bima na wastani wa faida ya muagiziaji wa mafuta (Premium), kwa mujibu wa Wakala wa Uagiziaji wa mafuta wa pamoja (Petroleum Bulk Procurement Agency (PBPA)).
- **Tatu,** thamani halisi ya shilingi ya Tanzania kwa kulinganisha na dola ya Marekani.
- **Nne,** tozo na ada mbali mbali zinazotozwa mafuta hayo katika Bandari ya Dar es Salaam kwa mafuta ambayo hayauzwi katika soko la ndani (Transit/Transhipment).
- **Tano,** gharama za kuhifadhi mafuta Tanzania Bara.
- **Sita,** gharama za kuyaleta mafuta Zanzibar (Back Loading)
- **Saba,** gharama za lazima zinazotozwa Bandarini Zanzibar.
- **Nane,** kodi na ada zinazotozwa na Serikali kwenye biashara ya mafuta.
- **Tisa,** kiwango cha faida wanachokipata wauzaji wa jumla na reja reja.


Ni ukweli usio na shaka, upo uhusiano wa bei za mafuta ghafi katika soko la dunia na bei za hapa nyumbani.

Mafuta ghafi hununuliwa katika soko la Dunia na kupelekwa kwenye viwanda vya kusafishia mafuta ili kupata mafuta safi. Hatua hii huchukua takriban miezi miwili au zaidi ili mafuta hayo yaweze kufika Zanzibar kwa ajili ya matumizi. Bei za mafuta hupangwa kwa kutumia gharama halisi za uagiziaji mafuta ambazo hutokana na kiwango kilicho ainishwa na mzabuni aliyeshinda kuleta mafuta kwa mwezi husika na kuthibitishwa na Mamlaka zinazosimamia uagiziaji wa mafuta, ambayo huwa yamenunuliwa mwezi wa nyuma yake.

Kwa mfano, Mamlaka zinazohusika na uagiziaji wa mafuta hutoa zabuni za Uingizaji wa mafuta yatakayotumika mwezi wa Januari katika mwezi wa Novemba, kwa kuzingatia hali halisi.

Hivyo, uhusiano wa bei za soko la dunia na soko la Zanzibar kwa mafuta safi hupishana kwa miezi miwili.

Hii, inamaanisha kwamba kushuka kwa bei za mafuta katika mwezi wa Novemba, athari yake itaonekana katika soko la Zanzibar katika mwezi wa Januari.



# ZURA

## Kujenga Ofisi mpya za kisasa




Mchoro unaoonesha majengo mapya ya Makao Makuu ya ZURA na Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati litakavyokuwa baada ya kazi za ujenzi wa majengo hayo utakapokamilika.

**Na Khuzaimat Bakar**

**HIVI** karibuni, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) inatarajia kupata majengo ya uhakika yanayolingana na shughuli zake. Majengo hayo yamo katika hatua ya ujenzi unaofanyika Maisara katika eneo lililo karibu na jengo la Maktaba Kuu, Zanzibar.

Hivi sasa hatua kadhaa za ujenzi huo zimekamilika, ikiwemo kukamilisha michoro kupata mkandarasi na tayari majengo pacha yenye ghorofa zisizopungua sita (6) kila moja yamesimama katika eneo hilo.

Pamoja na ofisi za ZURA, sehemu ya majengo hayo yatatumika pia kwa ajili ya ofisi za Wizara inayosimamia ZURA.

Ujenzi wa ofisi za ZURA ni sehemu nyengine inayoangaliwa kuwa ni mafanikio makubwa ya utekelezaji wa mipango ya Serikali ya awamu ya saba chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein.

Itakumbukwa kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Kwa muda mrefu haikuwa na utamaduni wa ujenzi wa ofisi za serikali na ofisi nyingi zilizokuwa zikitumika zilirithiwa kutoka katika majengo yaliyokuwa ofisi enzi za ukoloni au nyumba za kuishi ambazo mara baada ya Mapinduzi ya Januari, 1964 zilitaifishwa na kuwa mali ya serikali.

Hali hiyo imeanza kubadilika kuanzia miaka ya 2000 na kupata kasi zaidi mwaka 2010, ambapo Serikali imeendelea na jitihada za makusudi za kujenga ofisi za kisasa zenye hadhi inayolingana na Serikali yenyewe. Miongoni mwa majengo mapya makubwa ya Serikali ni

pamoja na Wizara ya Utumishi na Utawala Bora na Bodi ya Mapato Zanzibar ambayo yapo mazizini. Majengo mengine ya kisasa ni Ofisi za Wizara mbali mbali za serikali zilizoko Gombani Pemba.

Katika nchi za ukanda wa kusini mwa jangwa la Sahara kumesheheni majengo yenye hadhi yanayotumiwa na ofisi za serikali, majengo hayo pamoja na kubeba dhana nzima ya utendaji wa serikali kutokana na muonekano wake, lakini pia hutumika kwa ajili ya kutoa haiba nzuri ya mji.

Miji kama Nairobi, Kampala, Kigali, Windhoek, Lusaka, Maputo na mingine inayo majengo makubwa yenye hadhi ya kitaifa na mataifa ambayo yanatoa taswira nzuri kwa ofisi za serikali zilizomo katika majengo hayo.

Ofisi zenye hadhi humjengea mtu imani na hujisikia mwenye faraja kutembelea katika ofisi hizo akiamini kwamba mahali hapo panatendwa kazi yenye tija na maslahi ya taifa kutokana na mandhari ya utulivu na rafiki katika utendaji kazi.

Uwepo wa majengo ya kisasa kwa wizara za serikali kuna punguza usumbufu wa utendaji kazi kwani taasisi zote zilizomo chini ya wizara husika zinapata nafasi ya kuwa pamoja na kurahisisha utendaji kazi.

ZURA inahitaji kuwa na majengo ya uhakika kutokana na majukumu iliyokabidhiwa na taifa. Ina mamlaka makubwa ya kiutendaji kwa kuwa inashika dhamana nyeti kwa ajili ya maendeleo ya taifa ya udhibiti wa huduma za maji na nishati.

Kimtazamo, taasisi nyeti kama hii inahitaji kuwa na majengo yenye hadhi kubwa na ofisi yanayolingana na hadhi na majukumu mazito iliyokabidhiwa. Kutokana na hali hiyo, ndio kulikopelekea ZURA kuamua kuwa na ofisi zinazolingana na hadhi yake.

Kwa mujibu wa majukumu na hadhi ya ZURA, kuwa na majengo bora na ya kisasa sio suala la anasa, bali ni jambo la lazima ambalo linahitaji mkakati imara utakaochangia ufanisi katika utendaji wa kazi za kila siku.

Kwa mfano, suala la udhibiti na

Wafanyakazi wa ZURA wakiwa katika picha ya pamoja mbele ya jengo jipya la ofisi yao baada ya kumalizika hatua za uwekaji wa msingi wa jengo hilo linalojengwa hapo Maisara, mjini Unguja





Pichani ni hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa jengo la ofisi ya ZURA na Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati lilioko eneo la Maisara Zanzibar

mwenendo wa mafuta Zanzibar, jambo hili linaifanya ZURA kushughulika na wafanyabiashara ya mafuta ambao kimaumbile ya utekelezaji wa biashara hiyo inahusisha makampuni na matajiri wakubwa wa ndani na nje nchi wenye kuhitaji mazingira maalumu ya kuwashughulikia kiutendaji.

Wanafalsafa wanaweka bayana kwamba unapozungumzia makampuni makubwa au matajiri wenye mamlaka, lazima ulingane na hadhi ya kundi hilo, vyenginevyo utakuwa dhaifu na utashindwa kutekeleza majukumu yako. Hili halina ubishi kwani waendesha biashara ya mafuta duniani kote ni matajiri wakubwa na ni kundi lenye hadhi. Katika hili lazima sehemu wanayokwenda kuzungumza na kupanga mikakati lazima iwe inayolingana na hadhi yao.

Sambamba na hilo, ZURA sasa imekuwa ikitambulika kimataifa baada ya kuwa mwanachama wa jumuia ya wadhibiti wa huduma za maji na usafi wa Mazingira kwa nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAWAS) inayoundwa na nchi za Kenya, Zambia, Msumbiji, Lesotho, Rwanda na Tanzania.

Aidha, ZURA ni mwanachama wa Jumuiya ya Wadhibiti wa Nishati kwa nchi za Afrika Mashariki (Energy Regulators Association of East Africa - EREA). Katika hatua kama hii, ZURA itakuwa inaalika na kualikwa katika mikutano na makongamano mbali mbali yatakayofanyika katika nchi hizo wanachama, pia wanachama watapata nafasi ya kutembelea ofisi za taasisi hizo katika nchi husika. Hii ndio kawaida katika jumuia za kikanda za mashirikiano.

ZURA nayo itakuwa na nafasi ya kuwaalika ama wanachama kuichagua Zanzibar kuwa mwenyeji katika baadhi ya shughuli zao za kikanda. ZURA bila ya ofisi inayolingana na hadhi yake itashindwa kuwaweka wageni wake mahala panapolingana na hadhi zao.

Ujenzi na ukamilishwaji wa majengo mawili ya ghorofa sita utaijengea Zanzibar heshima kubwa pamoja na ZURA kwa kuwa na majengo ya uhakika yanayolingana na hadhi na utendaji kazi wa kila siku za taasisi hiyo.



Wajumbe wa Bodi ya ZURA wakitembelea eneo litakalojengwa chelezo na kituo kikubwa kipya cha kuhifadhia mafuta huko Mangapwani/ Bumbwini, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

# Zanzibar kujenga hifadhi mpya ya mafuta

**Na Hassan Amour**

**KATIKA** uendelezaji wa biashara ya mafuta, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) imeazimia kuanzisha mradi mkubwa wa ujengaji wa chelezo na kituo kipya kikubwa cha kuhifadhia mafuta huko Mangapwani.

Mradi huo utatoa mwanga wa maendeleo ya Zanzibar kwani taasisi mbali mbali na vyombo vya baharini vitaweza kutumia chelezo (gati ndogo) ya meli za mafuta kitakachorahisisha upakuzi na upakizi wa mafuta yanayoingia na kutoka Zanzibar.

Mamlaka husika zinapaswa kukaa pamoja na kuhimiza upatikanaji wa rasilimali katika kuweza kufanikisha ujenzi wa chelezo hicho kwa haraka zaidi na kwa uhakika.

Eneo hilo lenye ukubwa usiopungua hekta 380 limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa chelezo hicho pamoja na matangi ya kuhifadhia mafuta na gesi asilia.

Eneo lililochaguliwa huko Mangapwani/Bumbwini Wilaya ya Kaskazini 'B', kilomita 12 kutoka mjini Zanzibar limetengwa kukidhi wingi wa huduma zilizopo na zinazotarajiwa kuwepo katika eneo hilo.

Kijiografia eneo hilo lina kina kirefu cha maji ya bahari ambacho kitaruhusu ukubwa wa meli tofauti zilizojaa shehena kubwa za mafuta kuweza kutia gati katika chelezo hicho.



Pichani ni wawakilishi ya Kampuni Wijaye Karya ya Indonesia watembelea eneo litakakojengwa chelezo na kituo kipya cha kuhifadhia mafuta huko Mangapwani/ Bumbwini, Kampuni ni moja ya kampuni zinazoomba kukubaliwa tenda zao kwa ajili ya ujenzi huo.

Ardhi ya eneo hilo tayari imeshafanyiwa tathmini ya kimazingira na kugundulika kuwa litaweza kuhimili mikikimikiki ya athari za mafuta ambayo hayataweza kuathiri kiasi kikubwa cha mazingira katika eneo hilo.

Eneo hilo limechaguliwa pia kuwa ni kiungo muhimu kwa meli na vyombo mbalimbali vitakavyochukua na kusafirisha mafuta kutoka na kuingia Zanzibar.

Aidha, eneo hilo liko karibu sana na kisiwa cha Pemba, bandari ya Tanga na Mombasa ambako shughuli mbalimbali zinazohusiana na usafirishaji wa mafuta zinatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Kwa vyovyote, eneo hili ni muhimu katika maendeleo ya Zanzibar kutokana na eneo linalotumika hivi sasa kwa uhifadhi wa mafuta kuwa dogo na kushindwa kuhimili kasi kubwa ya matumizi ya mafuta kwa Zanzibar.

Sambambana na hilo, eneo la Mtoni linalotumika sasa kwa uhifadhi wa mafuta, limekuwa katikati ya mji na limezungukwa na nyumba nyingi wanazoishi watu na zinazotoa huduma za ustawi wa jamii. Hiyo, usalama katika eneo hilo ni tete.

Hifadhi ya mafuta iko karibu na maisha ya binaadamu. Hali hii haikubaliki katika nyanja za maendeleo na ustawi wa jamii kwani lolote linaweza kutokea katika hifadhi ya mafuta na kuweza kusababisha janga kwa taifa.

Zaidi ya watu 10,000 wanaishi katika eneo la Mtoni ambako mafuta ya Zanzibar kutoka sehemu mbali mbali yanahifadhiwa. Athari ya kimazingira kwa wanaoishi katika eneo hili haionekani kuwa ni salama; ijapokuwa ni mapema



kufikiria hilo lakini sio vibaya kusema kwamba hata hewa wanayovuta wengi wanaoishi katika eneo hilo pia inaweza kuwa sio salama.

Watafiti mbali mbali wanaeleza kuwa hewa inayoambatana na mafuta si vyema kutumiwa ama kuvutwa na binaadamu. Hewa hiyo inakuwa na mchanganyiko wa kemikali ambazo zinaweza kusababisha madhara makubwa kwa afya za binaadamu.

Karibu na eneo hilo, ipo hoteli ya nyota tano ya Mtoni Marine inayojengwa na kumilikiwa na Azam Group Company ambayo inaweza ikashindwa kufanya kazi ipasavyo ikiwemo kupokea wageni wa kimataifa kutokana na kuzungukwa na matangi ya hifadhi ya mafuta.

Pindi ZURA wakiweza kufanikisha mpango mkubwa wa ujenzi wa chelezo katika eneo hilo, mafuta yanayoingia Zanzibar yataweza kupata hifadhi salama na yenye kiwango. Nchi nyingi duniani zimekuwa zikipakua na kuhifadhi mafuta nje ya mji ili kuweza kuepusha majanga yasiyokuwa ya lazima.

Zanzibar nayo ikiwa ni sehemu ya dunia imeligundua hilo na kuamua kuandaa mkakati wa kuweza kuondoka na kuondoa hifadhi ya Mtoni kuelekea Mangapwani ambako mradi mkubwa wa matangi ya kuhifadhia mafuta pamoja na chelezo unatarajiwa kuanza kujengwa hivi karibuni.



Wawakilishi ya Kampuni Wijaye Karya ya Indonesia wakijieleza na kutambulisha uwezo wao watendaji wa ZURA ikiwa ni sehemu ya kutaka kukubaliwa kujenga kituo cha kuhifadhiia mafuta huko Mangapwani

# ZURA kuondoa uchakachuaji wa mafuta



Chini ya usimamizi wa ZURA, inachukuliwa sampuli ya mafuta yanayouzwa kwenye kituo cha mafuta kwa ajili ya kupima kiwango cha mafuta hayo ili kuthibitisha hakuna udanganyifu unaofanyika katika uuzaji wa mafuta hayo.

**Na Mwandishi Wetu**

**KATIKA** kuendesha biashara ya mafuta, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), imejidhatiti kupambana na biashara haramu ya uchakachuaji wa mafuta inayoendeshwa na baadhi ya wafanyabiashara visiwani.

Kwa muda mrefu uchakachuaji wa mafuta umeonekana ni changamoto kubwa inayoikabili biashara ya mafuta Zanzibar kwani mafuta ya petroli yaliyochanganywa na dizeli au mafuta ya taa yamekuwa yakiharibu mashine nyingi kutokana na uchakachuaji huo kupoteza ubora na uhalisia wa mafuta.

Mamlaka imeiona changamoto hiyo na inaandaa mkakati maalum wa kutoa taaluma kwa waendesha biashara hiyo holela ya mafuta ili kuwanusuru na adhabu kubwa endapo wataingia hatiani kwa kutenda uovu huo.

Ni wazi kazi ya udhibiti wa biashara holela ya mafuta haiwezi kufanywa na ZURA pekee.

Hivyo, mipango mbali mbali imeandaliwa ya kuwakutanisha wadau kutoka sekta mbali mbali ambao watashirikiana kwa pamoja kuweza kulipatia ufumbuzi suala hili.

Faida itakayopatikana kutokana na udhibiti huu wa biashara holela ya mafuta pamoja na kudhibiti uchakachuaji wa bidhaa ya mafuta ni kuwa na bidhaa bora na yenye kiwango ambayo inaweza kutumika na kuwa na tija kwa taifa pamoja na watumiaji.

Sambamba na hatua hii taifa litaweza kujikusanyia kodi ya uhakika kutokana na biashara ya mafuta, kodi ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa katika ujenzi wa nchi hasa katika sekta mbali mbali ambazo zinahitajika kwa ajili ya maendeleo.

Kinachoonekana ni kuwa biashara holela ya mafuta inaweza kuondoka mara moja kwani vituo 'bubu' vya mafuta havitakuwa na ulazima kuwepo nchini kwa kuwa bidhaa ya mafuta inapatikana kwa uhakika na kwa bei yenye faida kati ya mfanyabiashara na mtumiaji.

Katika kukabiliana na uovu huo, ZURA inaandaa mfumo wa adhabu kwa wote ambao watakutwa na makosa dhidi ya kanuni na taratibu zilizowekwa kwa lengo la kuweka ufanisi katika shughuli za uendeshaji na udhibiti wa nishati ya mafuta nchini.

Wachunguzi kutoka nchi mbali mbali zenye taasisi zinazofanana na ZURA wametoa uzoefu wao kwamba kutokuwepo kwa adhabu kwa wanaokumbwa na hatia ya kushindwa kusimamia utekelezaji wa kanuni zilizowekwa, makosa yaliopo yataendelea na ZURA itakuwa sawa na 'mchunga' asiye na bakora.

Sheria zinaweka bayana aina tofauti za adhabu zinazoweza kutumika kwa watakaokumbwa na makosa ikiwemo za kupewa onyo, kusitishwa leseni pamoja na kufungiwa kufanya biashara ya mafuta kwa wale ambao watashindwa kutekeleza wajibu wao.



Zoezi la upimaji wa mafuta hufanyika kwenye kituo cha kuuzia mafuta kwa kutumia mashine ya kupimia mafuta hayo ambayo huchukuliwa kwenye gari kama inavyoonekana pichani

# ZURA mkombozi wa maji salama



Maofisa wa ZURa wakikagua kazi ya ukarabati wa bomba la maji lililopasuka Vikokotoni mjini Unguja ili kuhakikisha ukarabati huo unazingatia suala la upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi.

**Na Mwandishi Wetu**

MUHIMU wa maji kwa jamii unafahamika, lakini kuna haja ya kujenga taswira ya kuelewa kwamba hivi karibuni kumetokea uhaba mkubwa wa rasilimali hiyo duniani. Zanzibar ikiwa ni sehemu ya dunia nayo pia inakumbana kwa kiasi kikubwa na tatizo hilo la upungufu wa maji.

Kwa wale waliozaliwa katika miaka ya 1970 na kurudi nyuma, walishuhudia neema ya maji. Watoto wakiogelea katika mabwawa yaliyokuwa yamezagaa nchi nzima, mito ilikuwa imejaa kiasi ambacho watoto walikuwa wakizama na wengine kufa maji. Mifereji (mabomba) ilikuwa ikitoa maji safi na salama kwa uhakika. Mifereji hiyo ilikuwepo kwenye mitaa na nyumba za mijini na baadhi ya sehemu za vijijini.

Maji hayo yalikuwa yakitoka kwenye chemchem zilizojaa neema hiyo ya maji safi na salama iliyokuwa ikiwanufaisha wakazi wa mijini na vijijini. Madaraja katika sehemu mbali mbali yalikuwa yakipitisha na kutiririsha maji kwa mwaka mzima.

Sasa hali hii ni tofauti, mazingira yameharibika kwa kiasi kikubwa na maji yameanza na yanaendelea kuadimika katika sehemu mbali mbali za Zanzibar. Vyanzo vya maji vinaharibiwa na vyengine kupotoea kila uchao. Hata maji yanayopatikana hayana uhakika wa usalama wake.

Kukua kwa miji kunakotokana na kuongezeka kwa ujenzi wa viwanda na nyumba za kuishi watu hadi karibu na vyanzo vya maji kumepelekea kwa kiwango kikubwa kuharibiwa kwa vyanzo hivyo kunakosababisha maji kuchanganyika na takataka, kemikali na hata vinyesi vya wanyama na binadamu.

Maisha ya wananchi wengi yako hatarini kutokana na maji kuhusishwa kuwa ni chanzo kikubwa cha maradhi hasa maradhi hatari ya miripuko yanayopoteza maisha ya watu kwa urahisi zaidi.

Ili kukabiliana na hali hiyo, umuhimu wa kuwepo Mamlaka

ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) unajitokeza waziwazi katika kutekeleza wajibu wake wa kudhibiti ubora na kiwango cha maji.

Inakadiriwa Zanzibar ina watu millioni moja na nusu (1.5) wanaonufaika na huduma ya maji. Hii ni kutokana na makadirio ya ongezeko la watu la asilimia 3.5% kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002 ambayo ilionesha kuwepo watu 984,625. Wastani wa upatikanaji wa maji kwa Zanzibar ni asilimia 65% kwa makadirio ya saa 12 kila siku.

Idadi hii ya watu waliopo Zanzibar ni kubwa. Ni hatari iwapo idadi hiyo ya watu watakuwa wanaishi katika hali ya kubahatisha ya ukosefu wa maji safi na salama. Hakuna ubishi maisha ya watu hawa yatakuwa hatarini ikiwa huduma hiyo muhimu kwa jamii haiko salama.

Katika kuhakikisha kuwa maji yanakuwa salama kwa maisha ya binaadamu ZURA ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kuwa huduma za maji zinafikia kiwango kinachohitajika. ZURA inafanya kazi zake kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), bila ya kuwepo muingiliano au mgongano katika utekelezaji wa shughuli za taasisi hizo.

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ilianzishwa chini ya sheria ya Maji namba 4 ya mwaka 2006, ni taasisi iliyopewa majukumu ya kusimamia usambazaji wa maji pamoja na kusimamia vyanzo vyote vya maji ndani ya Zanzibar. ZURA kwa upande wake imepewa jukumu la kuhakikisha udhibiti wa maji kwa Zanzibar.

Udhibiti wa maji kwa ZURA ni hatua muhimu sana ambapo taasisi hiyo itahakikisha kuwa maji yanapatikana katika kila sehemu ya Zanzibar katika muda wote unaohitajika kwa matumizi ya binaadamu. La kuzingatiwa ni kuwa sio kusimamia upatikanaji wa maji tu, lakini maji hayo lazima yawe safi na salama katika matumizi ya viumbe hai.

Katika hili, ZURA itakuwa muwajibikaji wa usalama wa maji ya Zanzibar ili kuweza kufikia kiwango kinachohitajika kwa matumizi ya wananchi pamoja na kufikia kiwango cha kimataifa kwa lengo la kuwajengea imani watumiaji wa maji wa ndani na wanaokuja kutoka nje ya Zanzibar.

Hivyo, katika hili ZURA inawajibika kutoa leseni ya kusambaza maji kwa ZAWA. Aidha, ZAWA nao wanawajibika kufuata masharti yote yaliyomo katika leseni ya usambazaji wa maji ambayo itakuwa ikifanyiwa mapitio kila baada ya muda.

ZURA ina wajibu wa kuikagua ZAWA na kujiridhisha kuwa maji yanayosambazwa ni safi na salama na wala sio chanzo ama kichocheo cha maradhi ama tishio kwa maisha ya binaadamu. ZURA inawajibika kupita na kufuatilia katika kila chanzo cha maji na kuyapeleka maabara kuangalia ubora na usalama wake.

Iwapo ZAWA itashindwa kuwajibika kwa hili na kugundulika kuwa maji ya Zanzibar sio safi na salama katika kiwango kinachohitajika, ZURA itakuwa na wajibu wa kuichukulia hatua ZAWA za kushindwa uwajibikaji ikiwemo kunyang'anya leseni ya usambazaji maji Zanzibar.

Kuwepo kwa ZURA katika udhibiti wa maji Zanzibar haumaanishi kuinyima uhuru ZAWA, kilichopo ni ZAWA kuendelea na shughuli za kuhakikisha kwamba wanaendesha shughuli zao kwa kutekeleza malengo waliyopangiwa ikiwemo kuwataka wananchi kuchangia (malipo) katika maji ili kuimarisha huduma ya maji na kuhakikisha inapatikana kwa muda wote.

Hivyo, tegemeo kubwa la wananchi katika kusimamiwa usalama wao kutokana na matumizi ya maji liko kwa ZURA ambayo ina inabeba bango la ukombozi wa wananchi katika kudhibiti ubora na kiwango cha maji, kupanga tozo, ushuru na gharama za maji na pia kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa huduma hiyo kwa wakati wote.



Watendaji wa ZURA wakiangalia uungaji wa maji katika kijiji cha Kigunda, Kaskazini Unguja ili kuona iwapo uungaji huo umezingatia utaalamu kwa ajili ya kusimamia huduma ya maji salama.


ZURA